

# MKATABA WA KUPANGISHA OFISI

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 01/01/2024

KATI YA

MILKA DAVID MLAY WA S.L.P 2862 Dar es salaam (Ambaye hapa ni mmliki)

NA

UKWAYA TRADERS LIMITED S.L.P 55018 Dar es salaam (Ambaye hapa ni Mpangaji)

TAFADHALI SOMA MAELEZO YA MKATABA HUU KWA MAKINI KABLA YA KUKUBALIANA NAO. IWAPO HUWEZI KUTIMIZA MASHARTI YALIYOMO, TAFADHALI USISAINI.

1. Nimepanga nyumba/chumba/ofisi kwa gharama ya Tsh. 100,000/= (Laki moja tu.) kwa mwezi na jumla ya Tsh. 6,000,000/= Ambayo ni kodi ya miaka mitano (5) kuanzia tarehe 01/01/2024 hadi tarehe 01/01/2029 siku ambayo ndiyo ya mwisho ya mkataba wangu. Kama nitakuwa sijalipa kodi inayofuatia kutokana na makubaliano haya basi itakuwa ndio siku yangu ya mwisho ya kukaa kwenye ofisi hiyo, **Plot no.304** Sinza Mugabe Dar es salaam.
2. Usafi wa ndani ya ofisi lazima uzingatiwe. Malipo ya ubebaji taka, umeme na maji yatalipwa na mpangaji.
3. Bili za umeme na maji lazima zilipwe kila mwezi bila kupitiliza. Kushindwa kufanya hivyo ni kukiuka masharti ya mkataba hivyo mpangaji anaweza kulazimika kuondoka katika ofisi aliyopanga.
4. Mwenye ofisi atalazimika kukatisha mkataba kabla ya kumalizika endapo mpangaji atafanya mambo yafuatayo: -
  - a) Mpangaji anatabia ya kutoridhisha kwa wapangaji wengine kwa mfano kugombana ovyo na wapangaji wengine, kelele na fujo za aina yoyote ile, kutolipa ememe, maji au kufanya biashara yoyote kwenye ofisi bila idhini ya mwenye ofisi.
  - b) Kumpangisha mtu mwingine ofisi.
  - c) Kubomoa ofisi na kutengeneza bila maridhiano na mwenye ofisi.
5. Kodi
  - a) Kodi ikishalipwa hairudishwi
  - b) Kodi inaweza kupanda katikati ya mkataba na mpangaji atafahamishwa mwezi mmoja kabla ya mkataba kuisha.

Nimekubaliana na masharti ya mkataba huu


Sahihi ya mwenye nyumba

MILKA DAVID MLAY

Simu

0714-552878

Sahihi ya mpangaji



Simu

0715-598858